



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA NISHATI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA
HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI
(EWURA)



KUMB: PPR/2026 - 06/01

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA BIDHAA ZA MAFUTA YA
PETROLI KUANZIA JUMATANO, TAREHE 3 JUNI 2026**

Katika kuendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria, EWURA imeendelea kufuatilia mwenendo wa bei za mafuta katika soko la dunia na kupanga bei kikomo kwa mwezi Juni 2026.

Mabadiliko ya bei za mafuta nchini katika mwezi Juni 2026 yamechangiwa kwa kiasi kikubwa na vita inayoendelea eneo la Mashariki ya Kati, iliyoanza tarehe 28 Februari 2026, ikihusisha nchi za Marekani, Israeli na Irani. Vita hiyo imepelekea mashambulizi dhidi ya miundombinu muhimu ya uzalishaji, uhifadhi na usafishaji wa mafuta ikiwemo visima vya uzalishaji, maghala ya kuhifadhi na viwanda vya kusafisha mafuta na hivyo kuathiri uwezo wa uzalishaji na kusababisha upungufu wa mafuta katika soko la dunia kulikopelekea ongezeko la bei za bidhaa hiyo kwa kiasi kikubwa.

Aidha, kufungwa kwa Mlango Bahari wa Hormuz, ambao hupitisha takriban asilimia 20 ya mafuta yanayosafirishwa duniani, kumeathiri kwa kiasi kikubwa upatikanaji na usambazaji wa mafuta duniani na kuongeza gharama za usafirishaji pamoja na bima za meli za mafuta. Hali hiyo imepelekea kupungua kwa mzunguko wa meli, ambapo usafirishaji wa mafuta kupitia njia hiyo umeshuka kwa kiwango kikubwa na kusababisha msongamano wa meli, ucheleweshaji wa mizigo na kuongezeka kwa bei za mafuta katika soko la dunia.

Kwa kuwa Tanzania inaagiza sehemu kubwa ya mafuta yake kutoka nchi za Mashariki ya Kati, athari za mabadiliko hayo ya kimataifa zimejitokeza moja kwa moja katika soko la ndani.

Katika kukabiliana na hali hiyo, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuhakikisha mafuta yanapatikana nchini muda wote na kuendelea kuhakikisha bei zinaendelea kuwa himilivu ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza ikiwemo zile za kiuchumi na kijamii. **Miongoni mwa hatua hizo ni utoaji wa ruzuku ya takriban Shilingi 534.91 kwa kila lita moja ya mafuta ya dizeli.** Mafuta ya dizeli ni muhimu katika shughuli za kiuchumi na kijamii zikiwemo uzalishaji viwandani, usafirishaji wa bidhaa na huduma za usafiri wa umma.

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini zitakazotumika kuanzia **Jumatano ya tarehe 3 Juni 2026 saa 6:01 usiku.** Kwa mwezi Juni 2026, bei za rejareja na jumla katika Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga na Mtwara ni kama zinavyoonekana katika **Jedwali Na. 1 na 2, mtawalia.**

Jedwali 1: Bei Kikomo za Rejareja (Shilingi/Lita)

Bandari	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Dar es Salaam	4,086	4,333	4,685
Tanga	4,157	4,404	4,756
Mtwara	4,193	4,440	4,792

Jedwali 2: Bei Kikomo za Jumla (Shilingi/Lita)

Bandari	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Dar es Salaam	3,937.87	4,184.24	4,535.53
Tanga	3,940.03	4,176.17	--
Mtwara	3,940.51	4,183.84	--

Bei za reja reja za bidhaa za mafuta ya petroli kwa maeneo mbalimbali ya miji, wilaya na mikoa ni kama zinavyooneshwa katika **Jedwali Na. 3**.

MWENENDO WA BEI ZA MAFUTA YALIYOSAFISHWA KATIKA SOKO LA DUNIA

Bei za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini zinazingatia gharama za mafuta yaliyosafishwa (*FOB*) katika soko la dunia kwa kuakisi gharama za soko la Uarabuni. Mvutano unaoendelea wa kijiografia na kisiasa katika Mashariki ya Kati umevuruga kwa kiasi kikubwa uthabiti wa masoko ya mafuta duniani. Bei za mafuta yaliyosafishwa katika soko la Uarabuni zilipungua kwa asilimia 2.63, na kuongezeka kwa asilimia 0.70 na 1.97 mwezi Aprili 2026 kutoka wastani wa dola za Marekani 122.36 kwa pipa, dola 186.58 kwa pipa na dola 189.51 kwa pipa mwezi Machi 2026 kwa petroli, dizeli na mafuta ya taa, mtawalia.

MWENENDO WA GHARAMA ZA UAGIZAJI

Mgogoro huo pia umevuruga usafirishaji wa mafuta kupitia Mlango wa Hormuz, njia muhimu ya usafirishaji inayohudumia karibu asilimia 20 ya biashara ya mafuta duniani na kusababisha ongezeko kubwa la gharama za uagizaji mafuta. Mwezi Juni 2026, gharama hizo kwa bidhaa za mafuta zilizopokelewa kupitia Bandari ya Dar es Salaam ziliongezeka kwa wastani wa asilimia 55.50 kwa petroli, asilimia 95.51 kwa dizeli, na hakuna mabadiliko kwa mafuta ya taa, na hakuna mabadiliko kwa bidhaa za petroli, dizeli na mafuta ya taa kwa Bandari ya Tanga na Mtwara.

VIWANGO VYA KUBADILISHA FEDHA ZA KIGENI

Gharama za mafuta (*FOB*) na gharama za uagizaji (*Premiums*) zinalipwa kwa kutumia fedha za kigeni ikiwemo Dola ya Marekani. Kwa bei za mwezi Juni 2026, wastani wa gharama za kubadilisha fedha za kigeni (*Applicable Exchange Rate*) zimeongezeka kwa asilimia 0.37.

Wafanyabiashara wa bidhaa za mafuta kwa rejareja wanatakiwa kuuza mafuta kwa bei zinazooneshwa katika **Jedwali Na. 3**. Aidha, wafanyabiashara wa bidhaa za mafuta kwa jumla wanatakiwa kuuza mafuta kwa bei zinazooneshwa katika **Jedwali Na. 2**. **Hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mfanyabiashara yeyote atakayekiuka AGIZO hili.**

EWURA inapenda kuwakumbusha wafanyabiashara wa bidhaa za mafuta ya petroli kwa jumla na rejareja, pamoja na jamii, kuzingatia yafuatayo:

- a) Bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli kwa eneo husika zinapatikana kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba *152*00# na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.
- b) Kwa mujibu wa **Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, kifungu namba 166**, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei hizo kikomo.
- c) Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani isipokuwa **bei hizo zisizidi bei kikomo (Price cap) au kuwa chini ya bei iliyoruhusiwa (Floor Price) kama zilivyokokotolewa kwa mujibu wa Kanuni za EWURA za Kupanga Bei za Mafuta za Mwaka 2022 zilizotangazwa tarehe 28 Januari 2022 kupitia Gazeti la Serikali Na. 57 na marekebisho ya Kanuni tajwa kupitia Gazeti la Serikali Na. 761A la tarehe 30 Oktoba 2023 na Mabadiliko ya Kanuni za Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja za Mwaka 2024.**
- d) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana yakionesha bei za mafuta, punguzo, vivutio vya kibiashara vinavyotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyoza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**
- e) Wauzaji wa bidhaa za mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa stakabadhi za mauzo kutoka kwenye *Electronic Fiscal Pump Printers (EFPP)* na wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo zitatumika kama ushahidi kwa wanunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora unaotakiwa. Stakabadhi hizo pia zitasaidia kurahisisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mauzo ya bidhaa za mafuta ya petroli.

JEDWALI Na. 3: Bei Kikomo za Rejareja – TZS/Lita

Na.	Mji	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
1	Dar es Salaam	4,086	4,333	4,685
2	Arusha	4,205	4,452	4,804
3	Arumeru (Usa River)	4,205	4,452	4,804
4	Karatu	4,223	4,470	4,822
5	Longido	4,216	4,463	4,815
6	Monduli	4,210	4,457	4,809
7	Monduli-Makuyuni	4,215	4,462	4,814
8	Ngorongoro (Loliondo)	4,296	4,544	4,895
9	Pwani (Kibaha)	4,100	4,347	4,699
10	Bagamoyo	4,107	4,354	4,706
11	Bagamoyo (Miono)	4,137	4,385	4,736

Na.	Mji	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
12	Bagamoyo (Mbwewe)	4,118	4,366	4,717
13	Chalinze Junction	4,110	4,357	4,709
14	Chalinze Township (Msata)	4,114	4,361	4,713
15	Kibiti	4,116	4,363	4,715
16	Kisarawe	4,103	4,350	4,702
17	Mkuranga	4,105	4,353	4,704
18	Rufiji	4,123	4,371	4,722
19	Dodoma	4,174	4,422	4,773
20	Bahi	4,182	4,429	4,781
21	Nagulo	4,183	4,430	4,781
22	Chamwino	4,170	4,417	4,769
23	Chamwino (Mlowa)	4,182	4,429	4,781
24	Dabalo	4,182	4,430	4,781
25	Chemba	4,201	4,448	4,800
26	Kondoa	4,207	4,455	4,806
27	Kongwa	4,172	4,419	4,771
28	Mpwapwa	4,176	4,423	4,775
29	Mpwapwa (Chipogoro)	4,188	4,435	4,787
30	Mtera (Makatopora)	4,193	4,441	4,792
31	Mvumi	4,181	4,428	4,780
32	Geita	4,311	4,558	4,910
33	Bukombe	4,295	4,542	4,894
34	Chato	4,332	4,579	4,931
35	Mbogwe	4,349	4,597	4,948
36	Nyang'hwale	4,326	4,573	4,925
37	Iringa	4,180	4,427	4,779
38	Ismani	4,185	4,432	4,784
39	Kilolo	4,184	4,431	4,783
40	Mufindi (Mafinga)	4,190	4,437	4,789
41	Mufindi (Igowole)	4,198	4,446	4,797
42	Mufindi (Mgololo)	4,202	4,449	4,801
43	Kagera (Bukoba)	4,361	4,609	4,960
44	Biharamulo	4,335	4,583	4,934
45	Karagwe (Kayanga)	4,378	4,625	4,977
46	Kyerwa (Ruberwa)	4,383	4,631	4,982
47	Muleba	4,354	4,601	4,953
48	Ngara	4,349	4,596	4,948
49	Misenyi	4,370	4,617	4,969
50	Katoro	4,371	4,618	4,970
51	Katavi (Mpanda)	4,293	4,541	4,892
52	Mlele (Inyonga)	4,275	4,522	4,874
53	Mpimbwe (Majimoto)	4,313	4,560	4,912
54	Tanganyika (Ikola)	4,311	4,559	4,910
55	Kigoma	4,303	4,550	4,902
56	Uvinza (Lugufu)	4,293	4,541	4,892
57	Muyobozi Village (Uvinza)	4,305	4,552	4,904
58	Ilagala Village (Uvinza)	4,308	4,555	4,906
59	Buhigwe	4,302	4,549	4,901
60	Kakonko	4,304	4,551	4,903
61	Kasulu	4,312	4,559	4,911
62	Kihungwe	4,337	4,584	4,936
63	Manyovu	4,309	4,557	4,908

Na.	Mji	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
64	Kibondo	4,310	4,557	4,909
65	Kilimanjaro (Moshi)	4,189	4,437	4,788
66	Hai (Bomang'ombe)	4,193	4,440	4,792
67	Mwanga	4,182	4,430	4,781
68	Rombo (Mkuu)	4,210	4,458	4,809
69	Same	4,176	4,423	4,775
70	Siha (Sanya Juu)	4,196	4,443	4,795
71	Lindi	4,175	4,422	4,773
72	Lindi-Mtama	4,193	4,440	4,792
73	Kilwa Masoko	4,140	4,387	4,738
74	Liwale	4,195	4,443	4,794
75	Nachingwea	4,204	4,451	4,803
76	Ruangwa	4,205	4,453	4,804
77	Manyara (Babati)	4,248	4,495	4,847
78	Hanang (Katesh)	4,259	4,506	4,858
79	Kiteto (Kibaya)	4,259	4,506	4,858
80	Mbulu	4,261	4,508	4,860
81	Simanjiro (Orkasumet)	4,280	4,527	4,879
82	Mara (Musoma)	4,314	4,562	4,913
83	Musoma Vijijini (Busekela)	4,327	4,575	4,926
84	Rorya (Ingirijuu)	4,321	4,569	4,920
85	Rorya (Shirati)	4,329	4,577	4,928
86	Bunda	4,301	4,548	4,900
87	Bunda (Kisorya)	4,318	4,566	4,917
88	Butiama	4,312	4,559	4,911
89	Serengeti (Mugumu)	4,323	4,570	4,922
90	Tarime	4,323	4,570	4,922
91	Tarime (Kewanja/Nyamongo)	4,329	4,576	4,928
92	Mbeya	4,238	4,485	4,837
93	Chunya	4,247	4,495	4,846
94	Chunya (Makongolosi)	4,253	4,500	4,852
95	Chunya (Lupa Tingatinga)	4,254	4,502	4,853
96	Kyela	4,254	4,501	4,853
97	Mbarali (Rujewa)	4,212	4,459	4,811
98	Rujewa (Madibira)	4,225	4,472	4,824
99	Rujewa (Kapunga)	4,222	4,469	4,821
100	Rungwe (Tukuyu)	4,247	4,494	4,846
101	Busokelo (Iwangwa)	4,256	4,503	4,854
102	Morogoro	4,131	4,378	4,730
103	Mikumi	4,146	4,394	4,745
104	Kilombero (Ifakara)	4,173	4,421	4,772
105	Kilombero (Mlimba)	4,196	4,443	4,795
106	Kilombero (Mngeta)	4,185	4,432	4,784
107	Ulanga (Mahenge)	4,184	4,431	4,783
108	Malinyi	4,194	4,442	4,793
109	Kilosa	4,149	4,396	4,748
110	Gairo	4,149	4,396	4,748
111	Mvomero (Wami Sokoine)	4,141	4,388	4,740
112	Mvomero (Sanga Sanga)	4,131	4,378	4,730
113	Turian	4,156	4,403	4,755
114	Mtwara	4,188	4,435	4,787
115	Nanyumbu (Mangaka)	4,242	4,489	4,841

Na.	Mji	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
116	Masasi	4,214	4,461	4,813
117	Newala	4,220	4,467	4,819
118	Tandahimba	4,213	4,461	4,812
119	Nanyamba	4,213	4,461	4,812
120	Mwanza	4,291	4,538	4,890
121	Kwimba	4,309	4,556	4,908
122	Magu	4,299	4,546	4,898
123	Magu (Mahaha Shishani)	4,306	4,553	4,905
124	Misungwi	4,285	4,533	4,884
125	Misungwi (Mbarika)	4,295	4,543	4,894
126	Sengerema	4,323	4,571	4,922
127	Ukerewe	4,350	4,598	4,949
128	Njombe	4,213	4,460	4,812
129	Luponde	4,219	4,467	4,818
130	Njombe (Kidegembye)	4,239	4,486	4,838
131	Ludewa	4,256	4,503	4,855
132	Makambako	4,205	4,453	4,804
133	Makete	4,249	4,496	4,848
134	Wanging'ombe (Igwachanya)	4,211	4,458	4,810
135	Rukwa (Sumbawanga)	4,314	4,561	4,913
136	Sumbawanga Rural (Mtowisa)	4,314	4,561	4,913
137	Kalambo (Matai)	4,321	4,568	4,920
138	Nkasi (Namanye)	4,327	4,574	4,926
139	Kabwe	4,342	4,589	4,941
140	Nkasi (Kirando)	4,337	4,584	4,936
141	Ruvuma (Songea)	4,259	4,506	4,858
142	Mbinga	4,272	4,519	4,871
143	Namtumbo	4,264	4,512	4,863
144	Nyasa (Mbamba Bay)	4,282	4,529	4,881
145	Tunduru	4,239	4,486	4,838
146	Kizuka	4,270	4,517	4,869
147	Shinyanga	4,267	4,514	4,866
148	Kahama	4,271	4,518	4,870
149	Burugwa	4,280	4,527	4,879
150	Kishapu	4,275	4,522	4,874
151	Ushetu (Nyamilangano)	4,283	4,530	4,882
152	Ushetu (Kangeme Village)	4,289	4,536	4,888
153	Salawe	4,280	4,528	4,879
154	Simiyu (Bariadi)	4,285	4,532	4,884
155	Busega (Nyashimo)	4,297	4,544	4,896
156	Itilima (Lagangabilili)	4,285	4,532	4,884
157	Maswa	4,278	4,526	4,877
158	Meatu (Mwanhuzi)	4,289	4,537	4,888
159	Singida	4,206	4,454	4,805
160	Iramba	4,218	4,466	4,817
161	Manyoni	4,191	4,438	4,790
162	Itigi (Mitundu)	4,206	4,454	4,805
163	Itigi (Rungwa)	4,225	4,473	4,824
164	Ikungi	4,202	4,449	4,801
165	Misigiri	4,219	4,466	4,818
166	Mkalama (Nduguti)	4,236	4,483	4,835
167	Songwe (Vwawa)	4,252	4,499	4,851

Na.	Mji	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
168	Songwe (Mkwajuni)	4,259	4,506	4,858
169	Ileje	4,256	4,503	4,855
170	Momba (Chitete)	4,261	4,509	4,860
171	Tunduma	4,256	4,504	4,855
172	Tabora	4,242	4,489	4,841
173	Igunga	4,242	4,489	4,841
174	Kaliua	4,255	4,502	4,854
175	Ulyankulu	4,252	4,500	4,851
176	Nzega	4,252	4,500	4,851
177	Sikonge	4,251	4,498	4,850
178	Urambo	4,252	4,499	4,851
179	Uyui	4,248	4,496	4,847
180	Mpyagula	4,274	4,521	4,872
181	Tanga	4,152	4,399	4,751
182	Handeni	4,131	4,378	4,730
183	Kilindi	4,166	4,413	4,765
184	Korogwe	4,145	4,392	4,744
185	Lushoto	4,154	4,402	4,753
186	Lukozi	4,160	4,407	4,759
187	Bumbuli	4,163	4,410	4,762
188	Mkinga (Maramba)	4,166	4,413	4,765
189	Muheza	4,152	4,399	4,751
190	Pangani	4,158	4,406	4,757

Gerald M. Maganga
KAIMU MKURUGENZI MKUU – EWURA